

Ni wakati gani unaofaa kuweka vipandikizi

- Baada ya kuhakikisha kwamba mwanamke hana ujauzito.
- Mara tu baada ya mimba kuharibika
- Mara tu baada ya kujifungua
- Wakati wowote mtumiaji anapohitaji kubadili njia nyingine za uzazi wa mpango

Mambo ya kuzingatia

- Mtumiaji anashauriwa kurudi kliniki
 - Anapokuwa na tatizo lolote linalohusiana na vipandikizi au unapohitaji ushauri.
 - Baada ya miaka mitatu au mitano kwa ajili ya kutoa kipandikizi/ vipandikizi.
- Ikiwa mtumiaji amepata maambukizi ya VVU au UKIMWI hana haja ya kutoa vipandikizi kabla hakijaisha muda wake.
- Vipandikizi viwekwe na vitolewe na mhudumu wa afya na usijaribu kutoa mwenyewe.
- Baada ya kuwekwa kipandikizi mtumiaji atapewa kadi yenye tarehe ya mwisho wa matumizi vipandikizi/ kipandikizi. Ni muhimu kuitunza kadi hii kwa uangalifu.

KUMBUKA

- **Vipandikizi havizuii maambukizi ya VVU na magonjwa yatokanayo na kujamiiana.**
Tumia kondomu kila unapotaka kujamiiana.
- **Vipandikizi vinaweza kutolewa wakati wowote mwanamke anapohitaji kutoa.**



Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

VIPANDIKIZI



UZAZI WA MPANGO MAISHA BORA, FAMILIA BORA



USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI




fhi360
THE SCIENCE OF IMPROVING LIVES

Vipandikizi ni nini?

Ni vipande vidogo vya plastiki mfano wa njiti ya kiberiti vyenye vichocheo vinavyofanana na vichocheo vya asili vya mwili wa mwanamke. Ni njia ya muda mrefu ya uzazi wa mpango.

Aina za vipandikizi

- Kipandikizi cha kijiti kimoja – hukinga mimba kwa muda wa miaka mitatu (3)
- kipandikizi cha vijiti viwili - hukinga mimba kwa muda wa miaka mitano (5)



Je Vipandikizi huwekwa wapi?

Vipandikizi huwekwa kwenye mkono sehemu ya juu, chini ya ngozi upande wa ndani. Vipandikizi huwekwa na kutolewa na mtaalamu wa afya.



Jinsi vinavyofanya kazi

- Huzuia yai lisipevuke.
- Husababisha ute mzito kwenye mlango wa kizazi na hivyo kuzuia mbegu za kiume kupita.

Faida za vipandikizi

- Vinazuia mimba kwa muda wa miaka mitatu hadi mitano kutegemea na aina ya vipandikizi.
- Havipunguzi ubora na wingi wa maziwa kwa mama anayenyonyesha.
- Huanza kufanya kazi ndani ya saa 24 baada ya kuwekwa
- Mtumiaji anaweza kupata mimba mara tu vinapotolewa.
- Vinafaa kutumiwa na wanawake wote pamoja vijana na akinamama wenye maambukizi ya virusi vya UKIMWI.
- Haviathiri tendo la kujamiiana.
- Ni nzuri na yenye usiri
- Uwekaji wake ni wa haraka
- Mama hahitaji kurudi mara kwa mara baada ya kuwekwa

Maudhi madogo madogo

Katika kipindi cha miezi michache ya mwanzo baadhi ya wateja hupata dalili zifuatazo:

- Mabadiliko katika mzunguko wa hedhi
 - o kutokupata hedhi
 - o kupungua kwa siku za hedhi
 - o kupata hedhi kidogo na kwa siku chache
- Kupata matone matone ya damu kabla ya siku za hedhi
- Matiti kujaa
- Maumivu kidogo ya kichwa
- Mabadiliko ya uzito wa mwili

Nani anayestahili kutumia Vipandikizi?

- Mwanamke yeyote aliye katika umri wa kuzaa; awe tayari amepata watoto au bado.
- Mwanamke anayependa kupumzika kwa muda mrefu bila ya kubeba mimba.
- Mwanamke aliyejifungua; kipandikizi kinaweza kuweka wakati wowote baada ya kujifungua
- Mwanamke anayeishi na VVU

Nani asiyestahili kutumia vipandikizi?

- Mwenye matatizo ya moyo au shinikizo la damu
- Kama una tatizo la kutokwa na damu